

KARUCO COLLEGE



Uongozi wa KKKT/ Dayosisi ya Karagwe unayo furaha kubwa kuwataarifu wadau wote kuwa chuo chetu cha KARUCO kimepata usajili na kinatangaza nafasi za masomo katika mwaka wa masomo 2018/2019 kwa ngazi ya cheti (Astashahada) na diploma (Stashahada) kama ifuatavyo:

1. Astashahada ya Kilimo Mjumuisho (Certificate in General Agriculture)
2. Astashahada ya teknolojia ya mawasiliano (Certificate in Information and Communication Technology - ICT)
3. Stashahada ya Kilimo Mjumuisho (Diploma in General Agriculture)
4. Stashahada ya teknolojia ya mawasiliano (Diploma in Information and communication Technology - ICT)

Sifa za Mwombaji

1. **Ngazi ya astashahada ya Kilimo mjumuisho:** Mwombaji awe na angalau "D" tatu za masomo ya sayansi kidato cha nne. Kati ya hayo somo la baiologia ni la lazima. Aidha Mwombaji awe na angalau "D" ya somo la Kiingereza.
2. **Ngazi ya Stashahada ya kilimo mjumuisho:** mwombaji awe angalau "E" moja na "S" katika masomo ya sayansi katika kidato cha sita; **au** awe amehitim mafunzo ya Astashahada ya Kilimo na Mifugo kwa GPA isiyopungua 2.0, na awe na angalau "D" tatu za masomo ya sayansi kidato cha nne likiwemo somo la Baiologia. Aidha D ya somo la Kiingereza ni ya lazima.
3. Ngazi ya Astashahada ya Teknolojia ya mawasiliano; mwombaji awe amefaulu masomo manne kwa kiwango cha "D" kidato cha nne likiwemo somo la Kiingereza.
4. **Ngazi ya Stashahada ya Teknolojia ya Mawasiliano;** mwombaji awe na angalau "E" moja na "S" **au** awe amehitim mafunzo ya Astashahada ya Teknolojia ya Mawasiliano, Computer Science au Business Information Technology. Aidha, awe na "D" nne kidato cha nne likiwemo somo la Kiingereza.

Masomo hayo yasiwe ya dini.

Fomu za maombi ya kujiunga na chuo zinapatikana chuoni Karuco, Lutheran Karagwe Hotel, Nyumba ya Vijana Nkwenda, majimbo yote ya K.K.K.T/ Dayosisi ya Karagwe na kwenye tovuti ya Chuo (www.karuco.ac.tz) na ya dayosisi (www.karaqwe-diocese.org)



Karo zetu ni nafuu na zinalipwa kwa awamu.

Kwa maelezo zaidi fika Chuoni KARUCO au wasiliana nasi kwa nambari za simu zifuatazo: 0684 94 64 34, 0754 24 88 20 au 0756 84 97 84; au kwa barua pepe: info@karuco.ac.tz au principal@karuco.ac.tz